**kustahimili, mtendapo dhambi na kupigwa makofi? Lakini kustahimili, mtendapo mema na kupata mateso, huu ndio wema hasa mbele za Mungu. 2.21 Kwa sababu ndio mlioitiwa; maana Kristo naye aliteswa kwa ajili yenu, akawaachia kielelezo, mfuate nyayo zake.**

Tusisahau pia kwamba sheria hii ya kukataza kuabudu sanamu au miungu wengine bado ipo hata katika enzi hizi ijapokuwa iko katika mfumo tofauti; nchi nyingi bado zinatoa adhabu ya kifo kwa mtu yeyote anayehukumiwa mahakamani **kwa kosa la uasi au uhaini kwa serikali** iliyoko. Kosa hili ni la kukataa utawala ulioko na kukusudia utawala mwingine.

Somo hili linaelekezwa kwa wale wenzetu wanaojiona kuwa ni "watu walioendelea" au watu wa "kisasa au ki-leo" n.k. ambao wanasoma Biblia bila ufunuo wa Roho Mtakatifu (kwa sababu wanasoma wakiwa nje ya imani, ili kukosoa, sio kujifunza neno la Mungu) ambao wanaiona sheria hii ya Mungu ya kumpiga mawe hadi afe, mtu ambaye amemwasi Mungu, kuwa ni ya "kikatili" na ya "kizamani", haiendani na "nyakati za kisasa, za maendeleo."

Sasa, Wakristo wa leo hawajapewa amri hii ya kumwua anayefanya ibada ya sanamu, wala kumshitaki serikalini isipokuwa kumripoti kwa Kanisa ili atengwe mpaka atakapojirekebesha **(mfano: 1Wakorinto 5.1 Yakini habari imeenea ya kuwa kwenu kuna zinaa, na zinaa ya namna isiyokuwako hata katika Mataifa, kwamba mtu awe na mke wa babaye. 5.2 Nanyi mwajivuna, wala hamkusikitika, ili kwamba aondolewe miongoni mwenu huyo aliyetenda jambo hilo.**

MTU HUYU ALIAMRIWA NA MTUME PAULO ATENGWE; NA BAADAYE ANAREJESHWA KATIKA KUNDI.

**2Wakorinto 2:6-11 2.6 Yamtosha mtu wa namna hii adhabu ile aliyopewa na walio wengi; 2.7 hata kinyume cha hayo, ni afadhali mumsamehe na kumfariji, mtu kama huyo asije akamezwa katika huzuni yake ipitayo kiasi. 2.8 Kwa hiyo nawasihi kumthibitishia upendo wenu. 2.9 Maana naliandika kwa sababu hii pia, ili nipate bayana kwenu kwamba mmekuwa wenye kutii katika mambo yote. 2.10 Lakini kama mkimsamehe mtu neno lo lote, nami nimemsamehe; kwa maana mimi nami, ikiwa nimemsamehe mtu neno lo lote, nimemsamehe kwa ajili yenu mbele za Kristo, 2.11 Shetani asije akapata kutushinda; kwa maana hatukosi kuzijua fikira zake.)**

Hii ni kwa sababu taifa linalotawaliwa na Mungu Mwenyewe moja kwa moja katika nchi moja halipo tena, Hekalu halipo, na sisi wafuasi wa Mungu sio tena wafuasi kwa kuzaliwa katika taifa moja bali ni kwa KUZALIWA UPYA KATIKA KRISTO. Imani kwa Bwana Yesu ni chaguo-huru la kila mmoja wetu linalofanywa na kila mmoja wetu katika nchi anamoishi; hatutakiwi kutoa adhabu kwa mtu yeyote anayeamua



HAIJZWI

kutomwabudu Mungu, na kwa kweli Bwana Yesu anatufundisha tusimshawishi mtu yeyote kuja katika Imani kama hataki.

**Matayo 10:12-14: 12 Nanyi mkiingia katika nyumba isalimuni. 10.13 Na nyumba ile ikistahili, amani yenu na iifikilie; la, kwamba haistahili, amani yenu na iwarudie ninyi. 10.14 Na mtu asipowakaribisha wala kuyasikiliza maneno yenu, mtokapo katika nyumba ile, au mji ule, kung'uteni mavumbi ya miguuni mwenu.**

Katika jamii ya leo adhabu ya kifo haifanyiki waziwazi, mbele ya kadamnasi, hivyo watu wengi kwa kutosikia habari zake wanaiona kama kuwa ni ya kikatili wanaposikia kwamba mhalifu fulani amenyongwa; hii inatokana na UNAFIKI wa nafsi ambapo wanajali muonekano wa nje na kutoona au kusahau uhalisia wa matokeo ya maamuzi yetu ya hapa duniani katika ulimwengu wa kiroho AMBAO NDIO ULIMWENGU HALISI.

**Luka 11:37-40: 37 Alipokuwa akinena, Farisayo mmoja alimwita aje kwake ale chakula; akaingia, akaketi chakulani. 11.38 Farisayo huyo alipomwona, alistaajabu kwa sababu hakunawa kabla ya chakula. 11.39 Bwana akamwambia, Ninyi Mafarisayo mwasafisha kikombe na sahani kwa nje, lakini ndani yenu mmejaa unyang'anyi na uovu. 11.40 Enyi wapumbavu; aliyevifanya vya nje, siye yeye aliyevifanya vya ndani pia?**

Ndugu yangu, utaishi hapa duniani kwa miaka michache sana, lakini utaishi katika ulimwengu wa kiroho – peponi au motoni – MILELE! Matokeo ya ***maamuzi*** yako ya hapa duniani ndiyo utakayoishi nayo milele. Tafakari kwa hilo!

Yule mtu wa "kisasa, mpenda maendeleo, aliyestaarabika" anaiona adhabu hii kuwa ni kali kupita kiasi na watu hao wanapata picha kwamba Israeli ilikuwa nchi ya wafia-dini wapendao kumwaga damu, wanaoongozwa na Mungu mkatili! Lakini kwa kweli kweli kosa lile lilistahili adhabu hiyo na kama wana wa Israeli wangeitekeleza adhabu hii kikamilifu pale ilipoanza, taifa zima lisingeingia katika kushiriki kosa hili na Mungu asingeliangamiza taifa lake. Lakini historia inatuonyesha yaliyotokea – Israeli ilivamiwa na hawakuwa na uwezo wa kujitetea, kwani Mungu, mlinzi wao, aligeuza uso wake kutoka kwao. Ule ufalme imara uliotukuka aliouacha Mfalme Daudi na kisha Mfalme Solomoni umesambaratika, mpaka hapo Mwana wa Mungu mwenyewe atakapoiongoza tena Israeli kutoka Jerusalemu baada ya kumshinda mpinga-Kristo katika vita ya Armagedoni.

**Danieli 11:36-45: 36 Naye mfalme atafanya kama apendavyo; naye atajitukuza na kujiadhimisha juu ya kila mungu, naye atanena maneno ya ajabu juu ya Mungu wa miungu, naye atafanikiwa mpaka ghadhabu itakapotimia; maana yaliyokusudiwa yatafanyika. 37 Wala hatahijali miungu ya baba zake; wala yeye aliyetamaniwa na wanawake; wala hatamjali mungu awaye yote; maana atajitukuza mwenyewe juu**

